# MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI NOVEMBA, 2024 NA MWELEKEO KWA MWEZI DISEMBA, 2024.

**Dondoo za tathmini ya Novemba, 2024 na mwelekeo wa Disemba, 2024:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Novemba, 2024 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Disemba, 2024 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2024 vipindi vya mvua viliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka vipindi vya mvua vilijitokeza ikiashiria kuanza kwa mvua za Msimu, 2024/2025. Aidha, ongezeko la mvua lilijitokeza katika baadhi ya maeneo hususan katika wiki ya tatu na ya nne.

ii. Hali ya joto iliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan maeneo ya ukanda pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki katika kipindi cha Novemba 2024.

iii. Katika kipindi cha mwezi Disemba 2024, mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI NOVEMBA, 2024.


Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2024 vipindi vya mvua na ngurumo viliripotiwa katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka vipindi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ikiashiria kuanza kwa mvua za Msimu 2024/2025. Vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo machache na kusababisha mafuriko, upotevu wa maisha, uharibifu wa mali na kuathiri baadhi ya shughuli za kiuchumi. Kiwango cha juu

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 02/2023*

zaidi cha mvua cha milimita 91.7 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa Hendeni (Mkoa wa Tanga) mnamo tarehe 30 Novemba, 2024 ikifuatiwa na milimita 77.0 katika kituo cha Mwanza Marine (mkoa wa Mwanza) mnamo tarehe 20 Novemba, na milimita 73.7 katika kituo cha Ukiriguru (Mkoa wa Mwanza) mnamo tarehe 27 Novemba, 2024. Vituo vilivyopima mvua milimita 50 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba 1 hapo chini;




Kielelezo 1: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 50 au zaidi katika mwezi Novemba, 2024

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI DISEMBA, 2024

## 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Disemba, 2024 joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani, ikiashiria uwepo wa hali ya La Niña hafifu. Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa juu kidogo ya wastani, na eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupunguza kiasi upepo wenye unyevu unaovuma kuelekea ukanda wa pwani pamoja na mikoa ya jirani, na kuathiri mtawanyiko wa mvua. Hali ya joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani inatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango hafifu wa kusababisha upepo wenye unyevu kutoka misitu ya Congo kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Aidha, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa Afrika inatarajiwa kupungua nguvu kiasi na kupelekea Ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusogea taratibu kuelekea kusini.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI DISEMBA, 2024

Mvua zinatarajiwa kendelea katika maeneo mengi nchini katika kipindi cha Disemba, 2024. Hata hivyo, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini kutokana na kuimarika kwa Ukanda mvua. Kwa upande mwingine, hali ya joto inatarajiwa kuendelea kujitokeza hususan katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua zinayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya kwanza na ya pili.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Mvua zinayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Mvua zinazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Mvua zinazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Vipindi vya mvua zinayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza ya mwezi.

### 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI JANUARI, 2025

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2025 vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo.

### 2.4 USHAURI

Mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza. Hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Imetolewa tarehe 01 Disemba, 2024 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz